

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

**06**

**URAI A NA MAADILI**

**Muda: Saa 1:30**

**Mwaka 2021**

**Maelekezo**

1. Mtihani huu una sehemu A na B zenyé jumla ya maswali **sita (6)**
2. Jibu maswali **vote** katika kila sehemu.

**SEHEMU A (Alama 26)**

1. Jibu vipengele (i) – (v) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuandika katika kisanduku.
  - (i) Yapi kati ya yafuatayo ni makundi maalumu?
    - A. Wazee, watoto na walemavu
    - B. Watoto, matajiri na walemavu
    - C. Wafanyakazi, maalbino na wazee
    - D. Watoto, akinababa na walemavu[   ]
  - (ii) Ni tendo gani linaloonesha uwajibikaji wa watoto katika familia?
    - A. Kununua sare za shule
    - B. Kusaidia kazi ndogondogo za nyumbani
    - C. Kucheza mpira shulenii na nyumbani
    - D. Kujisomea muda wote[   ]
  - (iii) Mahitaji matatu ya msingi ambayo yanapaswa kutolewa na wazazi kwa watoto wao ni pamoja na:
    - A. Malazi, afya na ajira
    - B. Kitanda, chakula na ulinzi
    - C. Makazi, mkate na malazi
    - D. Chakula, mavazi na malazi[   ]
  - (iv) Gabo alaipokutana na Bibi kizee, alimsalimia na kumsaidia kubeba mzigo wake, tendo alilofanya Gabo ni kati ya matendo yanayoonesha nini?
    - A. Kumsaidia
    - B. Uadilifu
    - C. Wizi
    - D. Woga[   ]
  - (v) Pamela alitoa taarifa kwa mama yake kuwa alikuwa amevunja sahani. Tendo la kutoa taarifa alilofanya Pamela linaonesha tabia gani?
    - A. Kujipenda
    - B. Kuwa na upendo
    - C. Kuwa mkweli
    - D. Kuwa na huruma[   ]
2. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuoanisha maelezo kuhusu alama za Taifa katika Fungu A na alama husika kutoka katika Fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

| Fungu A  | Herufi | Fungu B             |
|--|--------|---------------------|
| (i) Alama inayowakilisha uhuru na nuru inayoangaza nchi yetu                       |        | A. Bendera ya Taifa |
| (ii) Alama yenyе rangi nne ambazo ni kijani, bluu, nyeusi na manjano.              |        | B. Fedha ya Taifa   |
| (iii) Alama inayoonesha picha ya mwanaamke na mwanaume upande wa kushoto na kulia. |        | C. Mwenge wa uhuru  |
| (iv) Alama inayoonesha uzalendo wa Taifa.  |        | D. Mnyama wa Taifa  |
|  |        | E. Nembo ya Taifa   |
|  |        | F. Wimbo wa Taifa   |

3. Jibu vipngele (i) – (ii) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.
- (i) Njia mojawapo ya kuhifadhi mazingira yetu ni \_\_\_\_\_  
(kukata miti, kuchoma misitu, kupanda miti)
  - (ii) Amani anatapika. Yawezekana anasumbuliwa na \_\_\_\_\_  
(maumivu ya mguu, ugonjwa wa malaria, ugonjwa wa ngozi)
  - (iii) Kunawa mikono kwa maji na sabuni kabla ya kula ni kitendo cha \_\_\_\_\_  
(uaminifu, kujijali, heshima)
  - (iv) Ili familia iweze kujipatia mahitaji yake muhimu inatkiwa kufanya nini?  
(kukata miti, kufanya kazi kwa bidi, kuhifadhi fedha benki)

### **SECTION B (Alama 24)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

4. Jibu vipengele (ii) – (v) kwa kujaza Kabilia au Mkoa ambao kabilia hilo hupatikana kwenye nafasi wazi katika Jedwali. Namba (i) imetolewa **kama mfano**.

| Na.   | Kabilia  | Mkoa     |
|-------|----------|----------|
| (i)   | Wapogoro | Morogoro |
| (ii)  | Wagogo   |          |
| (iii) |          | Mwanza   |
| (iv)  |          | Tabora   |
| (v)   | Wahaya   |          |

5. Chunguza picha ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.



**Maswali:**

- (a) wanafunzi kwenye hii picha wanafanya nini? \_\_\_\_\_
- (b) Unafikiri watoto hawa wapo katika mazingira yapi? \_\_\_\_\_
- (c) Ni faida ipi unayoweza kuipata unaposhiriki  
katika tendo lilioneshwa katika picha? \_\_\_\_\_
- (d) Taja jina la samani iliyopo pichani ambayo hutumiwa  
kuhifadhi vitabu. \_\_\_\_\_